

MLEVI AKISHALEWA

1. Mlevi akishalewa, apite barabarani
Haraka utamjuwa, kua pungufu kichwani
Azitupapo hatua, zote huenda pembeni
Mlevi akishalewa, humtii maanani.
2. Mlevi hana muruwa, heshima si yake fani
Maneno anayotowa, hayachukui uzani
Watamani kuyazoa, ukayatupe jaani
Mlevi akishalewa, humtii maanani.
3. Mlevi akibugia, pombe ijae tumboni
Ubabe atajitia, Kujifanya Taisoni
Na utundu huzidia, akawa ni kama nyani
Mlevi akishalewa, humtii maanani.
4. Ni simba hujidhania, anayetisha mwituni
Yu tayari kurukia, ndugu na wake jirani
Bila hata kutambua, analofanya ni nini
Mlevi akishalewa, humtii maanani.
5. Pesa atazochukua, ziwe tele mfukoni
Hapana itobakia, ya kurudisha nyumabani
Wanawe wanapolia, hajui awape nini
Mlevi akishalewa, humtii maanani.
6. Ulevi ukipungua, akapata ahueni
Haraka huangalia, imebaki pesa gani
Apate kuendelea, na wake ufirauni
Mlevi akishalewa, humtii maanani.
7. Sasa akikumbukia, hujihisi mtu duni
Kama kuku hubakia, hujinamia chini
Hawezi kuangalia, watu aliowahuni
Mlevi akishalewi, humtii maanani.
8. Kutahamaki hulia, kwa kuzidi tafrani
Lawana hujipakia, nimefanya kitu gani
Hutamani kukimbia, akajifiche mwituni
Mlevi akishalewa, humtii maanani.
9. Jamani wangu wasia, kwenu nyote ikhwani
Ulevi ni mbovu njia, inamhusu shetani
Epukeni nawambia, ulevi weka pembeni
Mlevi akishalewia humtii maanani.
10. Hapa kalamu natua, nimetoa ya moyoni
Ni bora kuzingatia, niliyotoa maoni
Na nazidi kukazia, ulevi msithamini
Mlevi akishalewa, humtii maanani.

Said bin Sultan
Box 256 pc 119
Oman
Said_almughairy@hotmail.com